BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

**BARAZA LA KUMI NA MOJA LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA PILI**

**Kikao cha Nne – Tarehe 16 Februari, 2026.**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua Itasomwa.

## I. MASWALI:

**Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

240. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Serikali ya Awamu ya Nane imebarikiwa kuwa na Makamu wa Pili wa Rais mchapakazi, mwenye uzoefu mkubwa wa utendaji kazi tokea akiwa Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa Mkoa na hatimae kuwa Makamu wa Pili wa Rais. Uchapakazi wake ni wa kupigiwa mfano.

(a) Kutokana na weledi wake wa utendaji wa shughuli za Serikali ndani ya Baraza, ni lini utaanzishwa utaratibu wa kuletwa maswali ya papo kwa papo kwa Makamu wa Pili, ili aweze kufafanua mambo yanayohitaji kauli ya Serikali ndani ya chombo hiki.

(b) Kwa kuwa Makamu wa Pili wa Rais ni mfuatiliaji mzuri wa kazi za Mawaziri na Serikali kwa ujumla, ni hatua zipi za kikanuni zitafanyika kumwezesha kutumia muda maalumu wa kushughulikia hoja muhimu za Wajumbe katika Baraza na kuzitolea majibu.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

19. MHESHIMIWA AZZA JANUARI JOSEPH (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Tunazipongeza kwa dhati Idara Maalum zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kazi nzuri inayoendelea ya ujenzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo katika visiwa vyetu.

a) Je, kuna posho maalumu wanazopatiwa askari hao kwa utekelezaji wa kazi za miradi ya maendeleo.

b) Je, ni kiwango gani cha fedha wanachopatiwa askari hao.

**Wizara ya Kazi na Uwekezaji:**

180. MHESHIMIWA SEIF HAMAD SULEIMAN (Jimbo la Ole) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi na Uwekezaji:

Kwa kuwa Sheria ya Ajira, Nambari 11 ya 2005 imeweka masharti ya ajira kwa wageni, ikiwa ni pamoja na kutangazwa ajira hiyo pale anapokosekana mtaalamu wa ndani kwenye eneo hilo. Vile vile, baada ya mgeni kuajiriwa, anatakiwa amfundishe mzawa kushikilia nafasi hiyo baada ya mkataba wake wa ajira kumalizika.

(a) Je, ni ajira ngapi zilizotangazwa baada ya kukosekana wazawa katika kipindi cha miaka mitano ya hivi karibuni na katika sekta zipi.

(b) Kwa kuzingatia takwimu rasmi za kila mwaka kwa miaka mitano ya hivi karibuni, je Serikali imepata mapato ya kiasi gani kwa kutoa vibali vya wafanyakazi kutoka nje ya nchi.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

93. MHESHIMIWA MOHAMMED ALI SALIM (Jimbo la Ziwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Ujenzi wa barabara kongwe ya Wete hadi Meli Tano uliathiri kwa kiasi kikubwa mabanda ya skuli ya Ziwani.

Je, lini Serikali itachukua hatua za dharura kumaliza ujenzi wa mabanda hayo ili kuondosha usumbufu kwa walimu na wanafunzi katika skuli hiyo.

123. MHESHIMIWA MARIAM SAID KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kumekuwa na tabia isiyoridhisha ya baadhi ya wananchi kuvamia maeneo ya majengo ya Serikali ikiwemo skuli na hospitali.

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga uzio katika skuli ya Uweleni.

**<u>Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:</u>**

85. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:

Waandishi wa Habari ni watu wenye mchango mkubwa katika kuleta maendeleo ya taifa lolote duniani. Hata hivyo, Waandishi hao hukosa nguvu kutokana na maslahi madogo ukilinganisha na kazi wanazozifanya.

(a) Je, Serikali ina mpango gani katika kuinua maslahi ya Waandishi wa Habari hapa nchini.

(b) Je, ni lini Serikali itatoa muongozo wa kiwango maalum cha malipo ya maslahi ya Waandishi wa Habari wa Serikali na wa Sekta Binafsi ili kulinda maslahi ya Waandishi hawa.

**<u>Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:</u>**

22. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Serikali ina mpango gani wa kuimarisha na kupanua mifumo ya umwagiliaji katika maeneo ya kilimo, ili kuhakikisha uzalishaji wa mazao unakuwa endelevu hata wakati wa ukame au mabadiliko ya tabianchi.

150. MHESHIMIWA ABDULWAHAB SAID ABUBAKAR (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Changamoto ya msimu wa uzalishaji mkubwa wa mazao na matunda kwa wakulima wa Zanzibar, inasababisha ongezeko la

bidhaa sokoni kwa wakati mmoja. Hali hii husababisha kushuka kwa bei, pamoja na hasara zinazotokana na uharibifu wa mazao, kutokana na upungufu wa miundombinu ya uhifadhi, usindikaji na masoko. Kitendo hiki kinaathiri moja kwa moja kipato cha wakulima na mchango wa sekta ya kilimo katika uchumi wa Zanzibar.

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza na kuimarisha upatikanaji wa masoko ya nje (Export Markets) kwa mazao na matunda ya wakulima wa Zanzibar.

(b) Je, Serikali imejipanga vipi katika kuwawezesha wakulima kuzalisha mazao na matunda yanayokidhi viwango vya ubora, usalama na afya vinavyotakiwa katika masoko ya nje.

## <u>Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi:</u>

127. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Wakati wa ujenzi wa barabara ya Wete (22.1 Km), walikuwepo wananchi wakiwemo wa jimbo la Mtambwe ambao waliingia katika kundi la waliostahiki kulipwa fidia ya nyumba na wengine fidia ya miti. Pamoja na juhudi za Serikali kulipa fidia za nyumba, bado wananchi hawajapata fidia ya miti iliyong’olewa wakati wa ujenzi wa barabara hiyo.

(a) Kwa ufahamu wa Serikali juu ya suala hili, ni wananchi wangapi bado hawajalipwa fidia zao kulingana na tathmini iliyoifanya.

(b) Je, ni lini Serikali itawalipa wananchi hawa fidia zao.

198. MHESHIMIWA KHAMIS MOHAMMED AMRAN (Jimbo la Mkoani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Ninaipongeza Serikali ya Awamu ya Nane kwa kujenga barabara za ndani katika maeneo mengi hapa Zanzibar.

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara za ndani katika jimbo la Mkoani.

**Wizara ya Afya:**

117. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Alhamdulilahi, Hospitali ya Micheweni imeshajengwa na imekamilika na tayari imeanza kutoa huduma zake.

(a) Je, ni lini uzio ulioanza kujengwa hospitalini hapo utakamilika.

(b) Je, ni sababu zipi zilizoikwamisha Serikali kutokuukamilisha uzio huo uliojengwa zaidi ya miaka miwili iliyopita.

149. MHESHIMIWA MIHAYO JUMA SULEIMAN (Jimbo la Mwera) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Watumishi wa Serikali ya SMZ wamekuwa wakikatwa kiasi cha asilimia fulani kutoka katika mishahara yao na kuchangia Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar, ambapo mapato hayo yanawawezesha watumishi hao pamoja na wategemezi kutibiwa katika hospital zozote zile nchini.

Kwa kufuata utaratibu wa rufaa, hivi karibuni watumishi wa SMZ wameanza kupigiwa simu kutoka kwa Maafisa wa Mfuko huo na kuwaambia kuwa kwa upande wa wategemezi wazazi kutakuwa na vifurushi vitatu ambapo A, B na C. Hivyo, mtumishi anapochagua kifurushi A na B mtegemezi mzazi ataweza kutibiwa hospitali yoyote ile ila anapaswa kuchangia kiasi kisichopungua shilingi 200,000/- nje ya mshahara wake na kama hatakuwa na uwezo wa kuchangia katika kifurushi A na B basi mtegemezi mzazi atawekwa katika kifurushi C ambapo kitamlazimisha kutibiwa katika hospital za Serikali tu.

(a) Je, suala hili lina ukweli gani.

(b) Je, upi utaratibu wa kisheria uliowekwa juu ya fursa wanazostahili wategemezi kwa mujibu wa sheria.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

40. MHESHIMIWA MAHMOUD SHINENI ALI (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Tatizo la upatikanaji wa maji safi na salama limekuwa kubwa katika jimbo la Chambani hasa katika vijiji vya Ukutini, Chwale, Tondooni,

Matele na Kwa Azzan Wambaa. Shida hiyo inasababisha adha na usumbufu mkubwa kwa wananchi wa vijiji hivyo na kuzuwa taharuki ya kupelekea kuibuka kwa magonjwa ya mripuko wa tumbo mara kwa mara.

(a) Ni lini Serikali italipatia suluhisho la kudumu tatizo hilo na kuwaondoshea wananchi shida hiyo ya maji.

(b) Je, Serikali itaitekeleza lini ahadi yake ya kuvifanyia ukarabati visima vya zamani vilivyopo kwenye maeneo ya Kwa Kichwa Ukutini na Kiembeni kwa Popo Chambani.

(c) Ni upi msaada wa dharura na wa haraka wa kupatikana maji safi na salama, ambao Serikali ipo tayari kuutoa kwa wananchi wa vijiji hivyo.

195. MHESHIMIWA SEIF HAMAD SULEIMAN (Mwakilishi Jimbo la Ole)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Hapo zamani, watendaji wa Shirika la Umeme la Zanzibar (ZECO) walikuwa na kawaida ya kupita majumbani na sehemu mbalimbali wanazotoa huduma ya nishati ya umeme na kusoma mita, ili kujua matumizi ya mteja alivyotumia na baadae mtumiaji hupatiwa bili yake. Hata hivyo, hivi sasa kumekuwa na mabadiliko mengi ikiwemo kutumia mita za kisasa ambazo unalipia umeme kwanza ndio unatumia.

(a) Je, Serikali imepata faida gani katika mabadiliko haya ya kimfumo yaliyofanywa na Shirika la Umeme la Zanzibar.

(b) Je, gharama za uendeshaji wa Shirika la Umeme la Zanzibar (ZECO) zimebakia vile vile au kuna tofauti ipi kabla na baada ya mabadiliko ya mfumo yaliyofanywa.

**<u>Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:</u>**

220. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Kumekuwa na tatizo la Mamlaka ya Mji Mkongwe kwenye suala la usimamizi wa hifadhi ya nyumba za Mji Mkongwe na badala yake Mamlaka imekuwa inashughulika kufanya biashara za maegesho na vibali vya ujenzi ambavyo vimepandishwa bei kutoka shilingi 150,000 mpaka 1,000,000.

(a) Je, Serikali haioni sasa muda umefika wa kuifanyia

marekebisho makubwa Mamlaka ya Mji Mkongwe, ili iendane na madhumuni yake ya msingi ya kuanzishwa kwake ya kulinda na kuhifadhi Mji Mkongwe badala ya kufanya biashara.

(b) Lini Serikali itaifanyia marekebisho Sheria ya Mamlaka ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mji Mkongwe, ili kutimiza azma ya uhifadhi wa Mji Mkongwe.

**Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji:**

7. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Vijana, Ajira na Uwezeshaji:

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza upatikanaji wa mitaji, mikopo na fursa za kiuchumi kwa wanawake wajasiriamali.

## II. HOJA ZA SERIKALI

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

Mjadala wa Hotuba ya Uzinduzi wa Baraza la Kumi na Moja la Wawakilishi iliyotolewa tarehe 10 Novemba, 2025 na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

**Zanzibar,**
**16 Februari, 2026.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA LA WAWAKILISHI, ZANZIBAR**